**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA NA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# TAARIFA YA MAANDALIZI YA UTEKELEZAJI WA ELIMU-MSINGI YA LAZIMA YA MIAKA 10

**TAREHE 18 JANUARI, 2026**

**TAARIFA YA MAANDALIZI YA UTEKELEZAJI WA ELIMU-MSINGI YA LAZIMA YA MIAKA 10** .......... 1

**1. Utangulizi** .......... 4

**2. Upangaji wa Majaribio** .......... 4

**2.1.1 Matokeo ya Upangaji wa Majaribio ya Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza Mwaka 2028** .......... 4

**2.1.2 Wanafunzi wa Makundi–rika Mawili Watakaojiunga na Kidato cha Kwanza Mwaka, 2028** .......... 5

**2.1.3 Idadi ya Wanafunzi Wanaotarajiwa Kupata Nafasi** .......... 5

**2.1.4 Wanafunzi Wanaotarajiwa kukosa Nafasi ya Kujiunga na Kidato cha Kwanza Mwaka 2028** .......... 5

**2.1.5 Kata zenye Wanafunzi kati ya 2,001 hadi 8,000** .......... 6

**2.1.6 Kata zenye Msongamano wa Wanafunzi kati ya 1,001 hadi 2,000** .......... 6

**2.1.7 Kata zenye Msongamano wa Wanafunzi kati ya 101 hadi 1000** .......... 6

**2.1.8 Kata zenye Wanafunzi kati 01 hadi 100** .......... 6

**3. Mahitaji ya Miundombinu (Madarasa, Matundu ya Vyoo na Maabara, Karakana) Katika Kata zenye Zidio la Wanafunzi** .......... 7

**3.1 Kata zenye Zidio la Wanafunzi kati ya 2,001 hadi 8,000** .......... 8

**3.2 Kata zenye Zidio la Wanafunzi kati ya 1,001 hadi 2,000** .......... 8

**3.3 Kata zenye Zidio la Wanafunzi kati ya 101 hadi 1000** .......... 8

**3.4 Kata zenye Zidio la Wanafunzi kati ya 01 hadi 100** .......... 8

**3.5 Mahitaji ya Madarasa Mkondo wa Amali** .......... 13

**3.6 Mahitaji ya Karakana** .......... 13

**4. Mahitaji ya Walimu** .......... 14

**4.1 Ajira za Walimu Mkondo wa Jumla** .......... 14

**4.2 Mahitaji ya Walimu wa Amali** ........ 15

**5. Gharama za Kuendesha Elimu ya Lazima** ........ 17

**5.1 Gharama za Ujenzi wa Madarasa na Matundu ya Vyoo** ........ 17

**5.2 Gharama za ujenzi wa maabara** ........ 17

**5.3 *Gharama za Ujenzi wa Karakana*** ........ 17

**5.4 Gharama za Ajira Mpya za Walimu Mkondo wa Jumla** ........ 17

**5.5 Gharama za Ajira Mpya za Walimu na Wakufunzi Mkondo wa Amali** ........ 18

**5.6 Gharama za Uendeshaji** ........ 18

**6. Njia za Ugharamiaji** ........ 19

**6.1 Kutumia Miundombinu na Rasilimali Nyingine za Elimu** ........ 19

**6.2 Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi kupitia mifumo ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi** ........ 20

**6.2.1 Mapendekezo kwa Uteuzi wa Mfumo ya Ubia (*Decision Rules*)** ........ 22

***7.* Mapendekezo ya Kipaumbele cha Afua kwa Kuzingatia Mtawanyiko na Msambao (Spatial distribution) wa Kiwango cha Msongamano wa Wanafunzi** ........ 23

**8. Hitimisho** ........ 23

## 1. Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (Toleo la 2023) pamoja na Mitaala iliyoboreshwa iliyoanza kutekelezwa rasmi kuanzia Januari 2024. Mojawapo ya mabadiliko makuu ya sera ni kupunguzwa kwa muda wa Elimu ya Msingi kutoka miaka saba (7) hadi miaka sita (6), na kuongeza muda wa elimu ya lazima kutoka miaka saba hadi miaka kumi (10).

Mabadiliko haya yanasababisha kuwepo kwa makundi–rika mawili (double cohort) ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2028, ambapo wanafunzi walio Darasa la Tano na la Sita mwaka 2026 wanatarajiwa kuhitimu elimu ya msingi mwaka 2027 na kuanza elimu ya sekondari kwa wakati mmoja. Hali hii ni ya mpito lakini ina athari kubwa katika mfumo wa elimu ya sekondari, hususan katika maeneo ya upatikanaji wa miundombinu, walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, pamoja na rasilimali za kifedha.

Kwa kuzingatia tathmini zilizofanyika kupitia upangaji wa majaribio wa wanafunzi, utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa, na ripoti za maandalizi ya mapokezi ya wanafunzi wa makundi–rika mawili, andiko hili limeandaliwa ili kutoa taswira ya pamoja ya utayari wa utekelezaji wa Elimu ya Lazima ya Miaka 10 kwa kipindi cha mpito cha miaka minne (2028–2031).

## 2. Upangaji wa Majaribio

Ili kukabiliana na athari za ongezeko hilo la wanafunzi, Serikali imefanya zoezi la upangaji wa majaribio ya wanafunzi wa makundi-rika mawili mwaka 2028 kwa lengo la kubaini uhalisia wa uwezo wa miundombinu iliyopo na changamoto za upatikanaji wa nafasi katika shule za sekondari. Aidha, upangaji wa majaribio ulilenga kupata takwimu sahihi za mtawanyiko na msongamano wa wanafunzi watakaojiunga na Kidato cha Kwanza mwaka, 2028 katika ngazi ya Kata, Halmashauri na Mkoa kwa ajili ya kuweka mipango madhubuti ya mapokezi ya makundi–rika mawili ya wanafunzi hao. Zoezi hilo lilifanyika mwezi Desemba 2025 kwa kushirikisha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Baraza la Mitihani la Tanzania, na lilihusisha wanafunzi wote waliosajiliwa kufanya Upimaji wa Darasa la Nne mwaka 2024 na darasa la tano mwaka 2025.

### 2.1.1 Matokeo ya Upangaji wa Majaribio ya Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza Mwaka 2028

Matokeo ya upangaji wa majaribio yanaonesha kwa uwazi pengo kati ya mahitaji halisi ya wanafunzi na uwezo wa miundombinu iliyopo. Pengo hilo linathibitisha kuwa bila hatua za

makusudi, upatikanaji (access) na ubora (quality) wa elimu ya sekondari unaweza kuathirika, hususan kwa wanafunzi wa maeneo yenye msongamano mkubwa.

### 2.1.2 Wanafunzi wa Makundi–rika Mawili Watakaojiunga na Kidato cha Kwanza Mwaka, 2028

Zoezi la upangaji wa majaribio, lilibaini kuwa jumla ya wanafunzi **3,021,177** wanaunda makundi–rika mawili yanayotarajiwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka, 2028. Kati ya wanafunzi hao, wasichana ni **1,578,223**, ambapo **780,590** walikuwa Darasa la Nne na **797,633** walikuwa Darasa la Tano. Aidha, wavulana ni **1,442,954**, wakiwemo **709,799** wa Darasa la Nne na **733,155** wa Darasa la Tano.

### 2.1.3 Idadi ya Wanafunzi Wanaotarajiwa Kupata Nafasi

Upangaji wa majaribio uliofanyika unaonesha kuwa wanafunzi **1,065,042** sawa na **35.3%** (wasichana **564,641** na wavulana **500,401**) watapata nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza katika shule za sekondari **5,344** za Serikali mwaka 2028. Upangaji umezingatia uwiano wa chumba kimoja cha darasa kuchukua wanafunzi 50 (1:50) katika miundombinu iliyopo hadi Desemba, 2025. Shule hizo zimegawanyika katika makundi matatu kama jedwali Na. 1 linavyoonesha.

**Jedwali Na.1: Shule na Idadi ya Wanafunzi Wanaotarajiwa Kupangwa katika Shule za Sekondari**

| Aina ya Sekondari | Idadi ya shule | Wav | Was | Idadi ya wanafunzi waliopangwa |
|---|---|---|---|---|
| Ufaulu wa Juu | 7 | 480 | 340 | 820 |
| Amali za Kihandisi | 28 | 2161 | 1,299 | 3,460 |
| Amali zisizo za Kihandisi | 2 | 0 | 130 | 130 |
| Bweni Kitaifa | 69 | 1991 | 4,364 | 6,355 |
| Shule Teule | 103 | 9025 | 9,805 | 18,830 |
| Kutwa | 5024 | 486,744 | 548,703 | 1,035,447 |
| **Jumla** | **5,233** | **500,401** | **564,641** | **1,065,042** |

### 2.1.4 Wanafunzi Wanaotarajiwa kukosa Nafasi ya Kujiunga na Kidato cha Kwanza Mwaka 2028

Jumla ya Wanafunzi **1,956,135** (wasichana **1,013,582** na wavulana **942,553**) wanatarajiwa kukosa nafasi katika shule za sekondari zilizopo katika Kata zao na Kata jirani endapo miundombinu ya Shule za sekondari itabaki kama ilivyo sasa. Takwimu hizo zinaonesha kundi la wanafunzi Wasichana ndilo litaathirika zaidi. **Rejea Kiambatisho Na. 2.**

Makadirio ya upangaji wa wanafunzi watakaokosa nafasi ya kujiunga kidato cha kwanza mwaka, 2028 yameainishwa katika makundi manne ili kuonesha changamoto za kimahitaji. Makundi hayo ni kama yafuatayo:

### 2.1.5 Kata zenye Wanafunzi kati ya 2,001 hadi 8,000

Kundi hili lina jumla ya Kata **60** zenye jumla ya wanafunzi **179,172**. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa katika Kundi hili Kata yenye wanafunzi **2,007** itahitaji jumla ya Vyumba vya Madarasa **41** na Kata yenye wanafunzi **7,828** itahitaji jumla ya vyumba vya madarasa **157**.

Kundi hili lina wastani wa wanafunzi **2,987** kwa kila Kata wanaotarajiwa kukosa nafasi ya kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2028. Idadi hii ya wanafunzi **2,987** ni sawa na vyumba vya madarasa **60** kwa kila kata kwa uwiano wa wanafunzi 50 kwa darasa (1:50) (**Kiambatisho Na. 3).**

### 2.1.6 Kata zenye Msongamano wa Wanafunzi kati ya 1,001 hadi 2,000

Kundi hili lina jumla ya Kata **253** zinazotarajiwa kuwa na jumla ya wanafunzi **335,725**. Uchambuzi unaonesha kuwa katika Kundi hili Kata yenye wanafunzi **1,003** itahitaji jumla ya Vyumba vya Madarasa **21** na Kata yenye wanafunzi 1,997 itahitaji jumla ya vyumba vya madarasa **40**. Kundi hili lina wastani wa wanafunzi **1,327** kwa kila Kata watakaokosa nafasi ya kujiunga na Kidato cha Kwanza 2028. Idadi hii ya wanafunzi **1,327** ni sawa na vyumba vya madarasa **27** kwa kila Kata kwa uwiano wa wanafunzi **50** kwa darasa (1:50) (**Rejea Kiambatisho 4).**

### 2.1.7 Kata zenye Msongamano wa Wanafunzi kati ya 101 hadi 1000


Kundi hili lina Kata **3,367** zinazotarajiwa kuwa na jumla ya wanafunzi **1,428,102.** Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa katika Kundi hili Kata yenye wanafunzi **100** itahitaji jumla ya Vyumba vya Madarasa **2** na Kata yenye wanafunzi **998** itahitaji jumla ya vyumba vya madarasa **20**. Kundi hili lina wastani wa wanafunzi **425** kwa kila Kata ambao watakosa nafasi ya kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2028. Idadi ya wanafunzi hao **425** ni sawa na vyumba vya madarasa **9** kwa kila Kata kwa uwiano wa wanafunzi **50** kwa darasa (1:50) (**Rejea Kiambatisho 5).**

### 2.1.8 Kata zenye Wanafunzi kati 01 hadi 100

Kundi hili lina Kata 205 zinazotarajiwa kuwa na jumla ya wanafunzi **13,136**. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa katika Kundi hili Kata yenye wanafunzi **02** itahitaji chumba kimoja cha darasa na Kata yenye wanafunzi **99** itahitaji jumla ya vyumba vya madarasa **02.**

Kundi hili lina wastani wa wanafunzi **65** kwa kila Kata ambao watakosa nafasi ya kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka, 2028. Idadi hii ya wanafunzi **65** ni sawa na vyumba vya madarasa **02** kwa kila Kata kwa uwiano wa wanafunzi **50** kwa darasa (1:50) (**Rejea Kiambatisho Na.6.)**

**Ramani Na.1: Mtawanyiko na Msambao wa Kiwango cha Msongamano wa Wanafunzi Waliokosa Nafasi katika Ngazi ya Kata kwa makundi manne**




Ramani hii inadhihirisha wazi kuwepo kwa **Kata 413 zenye mahitaji makubwa na ya haraka**, ambazo zinapaswa kupewa kipaumbele cha juu katika ujenzi wa miundombinu, ajira za walimu na matumizi ya mbinu mbadala ikiwemo kushirikisha sekta binafsi.

## 3. Mahitaji ya Miundombinu (Madarasa, Matundu ya Vyoo na Maabara, Karakana) Katika Kata zenye Zidio la Wanafunzi

Sehemu hii inaonesha maeneo yenye msongamano wa wanafunzi watakaokosa nafasi za kujiunga na Kidato cha Kwanza katika shule za sekondari zilizopo katika Kata zao. Mtawanyiko na msongamano wa wanafunzi hao, unaashiria mahitaji ya miundombinu katika Kata yalipo makundi-rika hayo kama ifuatavyo: makundi ya Wanafunzi 2,001 hadi 8,000, Wanafunzi 1,001 hadi 2,000, Wanafunzi 101 hadi 1,000 na Mwanafunzi 01 hadi 100.

### 3.1 Kata zenye Zidio la Wanafunzi kati ya 2,001 hadi 8,000

Takwimu zinaonesha kuwa jumla ya wanafunzi **179,172** wanapatikana katika Kata **60**. Kwa kuzingatia kigezo cha ujenzi wa miundombinu ya elimu kinachobainisha kuwa kila wanafunzi **50** wanahitaji darasa moja pamoja na matundu mawili ya vyoo, Kata hizi **60** zinahitaji jumla ya vyumba vya madarasa **3,609**, matundu ya vyoo **7,218** na vyumba vya maabara **958** (Rejea **Kiambatisho Na. 3).**

### 3.2 Kata zenye Zidio la Wanafunzi kati ya 1,001 hadi 2,000

Takwimu zinaonesha jumla ya wanafunzi **335,725** wanapatikana katika Kata **353**. Kwa kuzingatia viwango vya ujenzi wa miundombinu kuwa kila wanafunzi 50 wanahitaji darasa moja pamoja na matundu mawili ya vyoo, Kata hizi zinahitaji jumla ya vyumba vya madarasa **6,844**, matundu ya vyoo **13,688** na vyumba vya maabara **1,711** (**Rejea Kiambatisho Na. 4).**

### 3.3 Kata zenye Zidio la Wanafunzi kati ya 101 hadi 1000

Takwimu zinaonesha kuwa jumla ya wanafunzi **1,428,102** wanapatikana katika Kata **3,367**. Kwa kuzingatia viwango vya ujenzi wa miundombinu kuwa kila wanafunzi 50 wanahitaji darasa moja pamoja na matundu mawili ya vyoo hivyo, jumla ya vyumba vya madarasa **30,238**, matundu ya vyoo **60,476** na vyumba vya maabara **7,560** vinahitajika. Rejea **Kiambatisho Na. 5.**

### 3.4 Kata zenye Zidio la Wanafunzi kati ya 01 hadi 100

Takwimu zinaonesha kuwa jumla ya wanafunzi **13,136** wanapatikana katika Kata 205. Kwa kuzingatia vigezo vya ujenzi wa miundombinu kuwa kila wanafunzi 50 wanahitaji darasa moja pamoja na matundu mawili ya vyoo, Kata hizi zitahitaji jumla ya vyumba vya madarasa **356**, matundu ya vyoo **712** na vyumba vya maabara **89.** (Rejea **Kiambatisho Na. 6).**


**Jedwali Na. 2: Kata zenye Zidio la Wanafunzi kwa kuzingatia Makundi**

| Na. | Kundi la Kata (Idadi ya Wanafunzi) | Idadi ya Kata | Jumla ya Wanafunzi | Wastani wa Wanafunzi kwa Kata | Wastani wa Madarasa Yanayohitajika kwa Kata (1:50) | Kiwango cha Mahitaji ya Madarasa (Chini - Juu) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Kundi 1:** (2,001 – 8,000) | 60 | 179,172 | 2,987 | **60** | 41 – 157 |
| 2 | **Kundi 2:** (1,001 – 2,000) | 253 | 335,725 | 1,327 | **27** | 21 – 40 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | **Kundi 3:** (101 – 1,000) | 3,367 | 1,428,102 | 425 | **9** | 2 – 20 |
| 4 | **Kundi 4:** (1 – 100) | 205 | 13,136 | 65 | **2** | 1 – 2 |
| | **JUMLA** | **3,885** | **1,956,135** | - | - | - |

Uchambuzi huu wa kieneo unathibitisha kuwa **afua zilizolengwa kijiografia (spatially targeted interventions)** ndizo zitakazowezesha Serikali kupunguza gharama, kuharakisha utekelezaji na kuhakikisha usawa wa upatikanaji wa Elimu ya Lazima ya Miaka 10.

**Ramani Na.2: Mgawanyo wa Mahitaji Ngazi ya Halmashauri**





Ramani hii inaonesha mgawanyo wa mahitaji kwa kila Halmashauri kwa kujumlisha mahitaji ya Kata zake. Inabainisha Halmashauri zenye mahitaji makubwa zaidi, hususan Halmashauri za mijini na pembezoni mwa miji, ambazo zinahitaji afua za haraka kabla ya mwaka 2028. Halmashauri zinazoongoza ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 8**.

**Jedwali Na. 8: Halmashauri zenye Uhitaji wa Afua za Haraka Zaidi**

| Nafasi | Mkoa | Halmashauri | Kata zenye Uhitaji Mkubwa | Wanafunzi Zaidi ya1000 (Jumla) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam | Dar es Salaam CC | 20 | 33,285 |
| 2. | Dar es salaam | Temeke MC | 13 | 33,285 |
| 3. | Geita | Geita DC | 15 | 31,025 |
| 4. | Geita | Chato DC | 10 | 17,426 |
| 5. | Mwanza | Nyamagana MC | 8 | 22,307 |
| 6. | Pwani | Kibaha TC | 7 | 13,698 |
| 7. | Kigoma | Uvinza DC | 6 | 10,617 |
| 9. | Morogoro | Morogoro MC | 6 | 14,307 |
| 9. | Shinyanga | Shinyanga MC | 5 | 12,537 |
| 10. | Kagera | Bukoba MC | 5 | 10,001 |

Halmashauri hizi zinapaswa kupewa **kipaumbele cha kwanza katika mgao wa bajeti, ujenzi wa miundombinu na ajira za walimu**.

**Ramani Na.3: Mtawanyiko wa Kiwango cha Msongamano wa Wanafunzi katika Ngazi ya Mkoa**




Ramani hii inaonesha mahitaji makubwa ya miundombinu ya elimu kwa kuzingatia jumla ya wanafunzi waliobaki kwa kila Mkoa. Rangi nzito zinaonesha Mikoa yenye mkusanyiko mkubwa wa mahitaji, ikiwemo Dar es Salaam, Geita, Mwanza na Pwani. Ramani hii inatoa msingi wa maamuzi ya kimkakati ya kugawa rasilimali katika ngazi ya kitaifa.

**Jedwali Na. 9: Mikoa yenye uhitaji wa Afua za Haraka Zaidi**

| Nafasi | Mkoa | Kata zenye Uhitaji Mkubwa | Wanafunzi Zaidi ya 1000 (Jumla) |
|---|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam | 55 | 128,894 |
| 2. | Geita | 38 | 74,244 |
| 3. | Mwanza | 29 | 43,259 |
| 4. | Pwani | 20 | 32,460 |
| 5. | Shinyanga | 19 | 26,383 |
| 6. | Kagera | 16 | 22,513 |
| 7. | Kigoma | 15 | 20,821 |
| 9. | Simiyu | 14 | 19,609 |
| 9. | Morogoro | 13 | 18,131 |
| 10. | Mbeya | 12 | 15,930 |

## 3.5 Mahitaji ya Madarasa Mkondo wa Amali

Jumla ya madarasa **2,068** yatatengwa kwa ajili ya wanafunzi wa Mkondo wa Amali. Kati ya madarasa hayo, **687** ni ya amali za kihandisi na **1,381** ni ya amali zisizo za kihandisi. Aidha, idadi ya wanafunzi wa amali za kihandisi itakuwa **35,060** wakati wale wa amali zisizo za kihandisi itakuwa **47,320**, hivyo kufanya jumla ya wanafunzi wa Mkondo wa Amali kwa mwaka 2028 kuwa **82,380**. Kwa maana hiyo, mwaka 2028, asilimia **42.6** ya wanafunzi wote wa amali watakuwa wanasoma amali za kihandisi na **57.4** watakuwa wanasoma amali zisizo za kihandisi.

## 3.6 Mahitaji ya Karakana

Idadi ya wanafunzi wa amali za kihandisi ilikadiriwa kuwa itaongezeka kwa asilimia 10 kwa mwaka wakati wale wa amali zisizo za kihandisi walikadiriwa kuongezeka kwa asilimia 15 kwa mwaka. Aidha, kwa kila madarasa nane ya amali kunahitajika karakana moja. Hivyo, ili kupata idadi ya karakana inayotakiwa, idadi ya madarasa yatakayojengwa iligawanywa kwa nane. Idadi ya madarasa kwa mwaka ilikokotolewa kutokana na ongezeko la wanafunzi kugawanywa kwa uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa. Idadi ya Karakana za Amali za Kihandisi zinazohitajika kujengwa kwa uwiano wa wanafunzi 30 kwa darasa, ni **60** na zisizo za kihandisi ni **25**. Hivyo, jumla ya karakana zote zinazohitajika kujengwa ni **85** kwa kigezo cha wananfunzi 30 kwa darasa.

**Jedwali Na 2: Mahitaji ya Karakana**

| Mwaka | Amali za Kihandisi | Amali zisizo za Kihandisi | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Idadi ya Wanafunzi (30) | Idadi ya Wanafunzi (30) | |
| 2027 | 60 | 25 | 85 |

**Jedwali Na.3: Miundombinu inayohitajika kutolea Elimu ya Lazima mwaka 2028**

| Miundombinu | Idadi inayohitajika |
|---|---|
| Madarasa | 41,047 |
| Matundu ya Vyoo | 82,094 |
| Maabara | 10,318 |
| Karakana za kihandisi | 60 |
| Karakana Zisizo za kihandisi | 25 |

## 4. Mahitaji ya Walimu

Makadirio ya mahitaji ya walimu kimasomo yamekokotolewa kwa kuzingatia kwamba masomo ya Basic Mathematics, Business Studies, English, Kiswahili, Geography na Historia ya Tanzania na Maadili yatasomwa na wanafunzi wote. Aidha, somo la Biology litasomwa na asilimia 80 ya wanafunzi wakati masomo ya Physics, Chemistry na History yatasomwa na asilimia 70 ya wanafunzi wote. Masomo mengine yaliyosalia yamekadiriwa kusomwa na asilimia 10 ya wanafunzi wote. Ukokotoaji wa mahitaji ya walimu kimasomo pia umezingatia idadi ya vipindi kwa wiki kwa kila somo kama ilivyoainishwa katika mitaala iliyoboreshwa.

### 4.1 Ajira za Walimu Mkondo wa Jumla

Kwa uwiano wa wanafunzi 50 kwa kila darasa, jumla ya walimu Hii ina maana kwamba, jumla ya walimu **46,041** watahijika kuajiriwa mwaka 2028. Mchanganuo wa kimasomo unaonesha kuwa mahitaji ya ajira ni makubwa katika masomo ya *Business Studies*, *Basic Mathematics, English Language, Physics, Biology* na Kiswahili. Masomo ya Geography, History, Fasihi ya Kiswahili na English Literature hayatahitaji ajira mpya. Masomo mengine yote yaliyobaki ambayo yanahitaji ajira mpya ni chaguzi. Matokeo ya makadirio ya mahitaji ya walimu kwa wanafunzi wa makundi-rika mawili wa Mkondo wa Jumla yameoneshwa katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na 4:** ***Mahitaji ya Walimu kwa Uwiano wa 50***

| Somo | Idadi ya Wanafunzi kwa Darasa | |
|---|---|---|
| | **Mahitaji** | Upungufu* |
| | **Mwaka 2028** | **Mwaka 2028** |
| Basic Mathematics | 15,774 | 6,967 |
| Business Studies | 9,465 | 8,131 |
| English Language | 15,774 | 4,738 |
| Geography | 7,887 | (4,220) |
| Historia ya Tanzania na Maadili | 7,887 | 2,612 |
| Kiswahili | 12619 | (113) |

| | | |
|---|---|---|
| Biology | 8834 | 1096 |
| Chemistry | 7729 | (252) |
| History | 7729 | (4994) |
| Physics | 7729 | 1730 |
| Additional Mathematics | 946 | 934 |
| Agriculture | 1577 | 1166 |
| Arabic Language | 946 | 898 |
| Book Keeping | 1104 | 372 |
| Chinese Language | 946 | 904 |
| Computer Science | 1262 | 853 |
| Fine Art | 1262 | 1237 |
| Food and Nutrition | 1577 | 1483 |
| French Language | 946 | 813 |
| Literature in English | 631 | (914) |
| Music | 1,262 | 1,246 |
| Sports | 1,262 | 1,232 |
| Textiles and Dressmaking | 1,577 | 1576 |
| Theatre Arts | 1,262 | 1238 |
| Fasihi ya Kiswahili | 631 | (671) |
| **Jumla ya Mahitaji** | **118,622** | |
| **Ajira Mpya** | | **38,970** |

*****_Bila ajira za kufidia walimu watakaostaafu, kufariki au kuacha kazi_

## 4.2 Mahitaji ya Walimu wa Amali

Ili kupata mahitaji ya walimu wa Amali za Kihandisi, kila fani mahsusi ilihusishwa na wataalamu wa fani kuu yake. Kwa mfano, walimu wa *Electrical Installation* ni *Electrical Engineers*, walimu wa *Welding and Metal Fabrication* ni *Mechanical Engineers* na walimu wa *Field Crop Production* ni wataalamu wa *Agriculture* (**Kiambatisho Na.1**). Ukokotoaji wa mahitaji ya walimu kimasomo pia umezingatia idadi ya vipindi kwa wiki kwa kila somo kama ilivyoainishwa katika mitaala iliyoboreshwa na kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya wanafunzi kwa kila fani.

### 4.2.1 Mahitaji ya Walimu wa Amali za Kihandisi

Takwimu zinaonesha kuwa kwa uwiano wa idadi ya wanafunzi **30** kwa kila darasa, jumla ya ajira mpya za walimu wa amali za kihandisi itakuwa **644** mwaka 2028.

**Jedwali Na 5:** ***Mahitaji ya Walimu wa Mkondo wa Amali za Kihandisi****

| Fani | Waliopo | Uwiano wa wanafunzi 30 | |
|---|---|---|---|
| | | Mahitaji | Ajira Mpya |
| | | Mwaka 2028 | Mwaka 2028 |
| Computer Science and Information Technology | 680.5 | 785 | 104 |
| Electrical Engineering | 26 | 136 | 110 |
| Mechanical Engineering | 29 | 142 | 113 |
| Civil Engineering | 49.9 | 184 | 134 |
| Automotive Engineering | 20 | 170 | 150 |
| Electronics and Computer Engineering | 9 | 19 | 10 |
| Electronics and Computer Science | 7 | 30 | 23 |
| **Ajira Mpya** | | | **644** |

*****_Bila ajira za kufidia walimu watakaostaafu, kufariki au kuacha kazi_

### 4.2.2 Mahitaji ya Walimu wa Amali Zisizo za Kihandisi

Jumla ya ajira mpya za walimu wa amali zisizo za kihandisi itakuwa **493** mwaka 2028.

**Jedwali Na 6:** ***Mahitaji ya Walimu wa Mkondo wa Amali zisizo za Kihandisi****

| Fani | Waliopo | Uwiano wa wanafunzi 30 | |
|---|---|---|---|
| | | Mahitaji | Ajira Mpya |
| | | Mwaka 2028 | Mwaka 2028 |
| Clothing and Textile | 3.5 | 57 | 54 |
| Food Processing | 0 | 21 | 21 |
| Agricultural Production | 38 | 57 | 19 |
| Wood Processing | 2 | 17 | 15 |
| Bee Keeping | 0.5 | 14 | 14 |
| Aquatic Food Production and Processing | 3 | 9 | 6 |
| Hospitality and Tourism | 8 | 205 | 197 |
| Cosmetology | 0 | 24 | 24 |
| Creative Arts | 4.5 | 105 | 100 |
| Football Performance | 0 | 14 | 14 |
| Netball Performance | 0 | 14 | 14 |
| Track Event | 0 | 14 | 14 |
| **Ajira Mpya** | **0** | **553** | **493** |

*****_Bila ajira za kufidia walimu watakaostaafu, kufariki au kuacha kazi_

### 4.2.3 Ajira Mpya za Wakufunzi wa Karakana

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 pamoja na mitaala iliyoboreshwa inasisitiza kuwepo kwa wakufunzi (*workshop instructors*) watakaowasaidia walimu katika utoaji wa elimu ya amali kwa vitendo. Jumla ya ajira mpya za wakufunzi wa karakana fani za Kihandisi itakuwa **60** na fani zisizo za kihandisi itakuwa **25** kwa mwaka 2028.

**Jedwali Na. 7: Ajira Mpya Wakufunzi wa Karakana mwaka 2028**

| **Mwaka** | **Amali za Kihandisi** | **Amali zisizo za Kihandisi** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Wanafunzi/ Darasa | 30 | 30 | 30 |
| 2028 | 60 | 25 | 85 |
| **Jumla** | **60** | **25** | **85** |

## 5. Gharama za Kuendesha Elimu ya Lazima

### 5.1 Gharama za Ujenzi wa Madarasa na Matundu ya Vyoo

Gharama za ujenzi wa kila darasa zilikadiriwa kuwa Shilingi millioni 25 wakati kila tundu la choo lilikadiriwa kugharimu Shilingi milioni 2.2. Aidha, kila maabara ilikadiriwa kujengwa kwa gharama ya Shilingi milioni 50. Kwa uwiano wa wanafunzi **50** kwa darasa, gharama za ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo zitakazohitajika ni Shilingi **Bilioni 859.2**

### 5.2 Gharama za ujenzi wa maabara

Gharama za ujenzi wa maabara zitakuwa Shilingi Bilioni **182.7** kwa mwaka 2028.

### 5.3 *Gharama za Ujenzi wa Karakana*

Kwa karakana za amali za kihandisi, ilikadiriwa wastani wa gharama ya Shilingi Milioni **150** kwa kila karakana na kwa zile zisizo za kihandisi gharama hizo zilikadiriwa kuwa wastani wa Shilingi Milioni **100**. Takwimu zinaonesha kuwa kwa uwiano wa wanafunzi 30 kwa darasa, gharama zitakazohitajika katika ujenzi wa karakana za kihandisi mwaka 2028 ni Shilingi Bilioni **11.50** wakati zisizo za kihandisi zitagharimu kiasi cha Shilingi Bilioni **6.186** mwaka 2028.

### 5.4 Gharama za Ajira Mpya za Walimu Mkondo wa Jumla

Gharama za ajira mpya zilikadiriwa kuwa Shilingi Milioni **12** kwa mwaka (mshahara na stahiki zingine) kwa kila mwalimu. Ajira mpya za walimu mkondo wa jumla zitagharimu kiasi cha Shilingi Bilioni **467.6** mwaka 2028.

## 5.5 Gharama za Ajira Mpya za Walimu na Wakufunzi Mkondo wa Amali

Ili kupata makadirio ya mishahara ya walimu na wakufunzi wa fani za kihandisi, viwango vya mishahara inayolipwa kwa kada hizo na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) vilitumika. Mishahara ya walimu wa fani zisizo za kihandisi ilikadiriwa kuwa sawa na mishahara ya walimu wa Mkondo wa Jumla. Kwa kutumia utaratibu huu, gharama za ajira mpya kwa mwaka ilikadiriwa kuwa **Shilingi 21,600,000** (mshahara na stahiki zingine) kwa kila mwalimu wa fani za kihandisi, **Shilingi 12,000,000** kwa kila mwalimu wa fani zisizo za kihandisi na **Shilingi 10,800,000** kwa kila mkufunzi wa karakana.

Kwa muktadha huo, ajira mpya ya walimu na wakufunzi wa amali za kihandisi zitagharimu kiasi cha Shilingi Bilioni **14.56** mwaka 2028. Ajira mpya ya walimu na wakufunzi wa amali zisizo za kihandisi zitagharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni 6.186** mwaka 2028.

## 5.6 Gharama za Uendeshaji

Ongezeko la wanafunzi katika ngazi ya elimu ya Sekondari Hatua ya Chini litasababisha pia ongezeko la gharama za uendeshaji. Gharama hizo ni pamoja na ruzuku ya uendeshaji na utawala wa shule, ruzuku ya vitabu na gharama za upimaji na chakula. Aidha, inapendekezwa kuanzishwa kwa ruzuku mahsusi kwa ajili ya kuhudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum, ambao nao idadi yao itaongezeka.

Ruzuku ya utawala na uendeshaji wa shule imekadiriwa kuendelea kuwa Shilingi **12,500** kwa kila mwanafunzi wa kutwa kwa mwaka. Vilevile, Serikali inatarajiwa kuendelea kulipa moja kwa moja kwa Taasisi ya Elimu Tanzania shilingi **12,500** kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kwa ajili ya uchapishaji na usambazaji wa vitabu.Inapendekezwa pia kuwa ruzuku mahsusi kwa ajili ya kuhudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum ikadiriwe kuwa asilimia 0.25 ya jumla ya gharama ya uwekezaji (miundombinu na ajira) kwa kila mwaka.

Baraza la Mitihani la Tanzania limetoa makadirio ya wastani wa gharama za upimaji na utahini kwa wanafunzi wa kidato cha pili na cha nne wa **Shilingi 54,337.85** kwa kila mwanafunzi. Kati ya gharama hizo, Shilingi **26,288.59** zitapitia Baraza la Mitihani Tanzania na Shilingi **28,049.26** zitapitia OR-TAMISEMI.

Pamoja na gharama za mahitaji ya miundombinu na ajira za walimu, takwimu bainishwa zinaonesha kuwa gharama ya ruzuku ya uendeshaji na utawala wa shule, na uchapaji na usambazaji wa vitabu kwa wanafunzi wa makundi-rika mawili itakuwa **Shilingi Bilioni 126.0** kwa mwaka 2028, gharama za ruzuku mahsusi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum zitakuwa **Shilingi Bilioni 3.854** kwa mwaka 2028 na gharama ya ruzuku ya upimaji na utahini itakuwa **Shilingi Bilioni 99.24** kwa mwaka 2028.

Kwa msingi huo, jumla ya mahitaji yote ya gharama zinazohitajika kuendesha elimu ya Sekondari ya Chini mwaka 2028 ni **Shilingi Trilioni 1.771** (Jedwali Na.10)

**Jedwali Na.10: Muhtasari wa Gharama za Elimu ya Lazima Mwaka 2028**

| Uwiano wa Wanafunzi 50 Mkondo wa Jumla na Wanafunzi 30 Mkondo wa Amali | |
|---|---|
| **MAHITAJI (Sh.Milioni)** | **Mwaka** |
| **A. Mkondo wa Jumla** | **2028** |
| Walimu | 467,639 |
| Ujenzi wa Madarasa na Matundu ya Vyoo | 859,215 |
| Ujenzi wa Maabara | 182,659 |
| **Jumla Ndogo** | **1,509,513** |
| | |
| **B. Mkondo wa Amali** | ***2027*** |
| Ajira za Walimu- Amali za Kihandisi | 13,910 |
| Ajira za Wakufunzi - Amali za Kihandisi | 648 |
| **Jumla Ajira - Amali za Kihandisi** | **14,558** |
| Ajira za Walimu - Wasio wa Kihandisi | 5916 |
| Ajira za Wakufunzi - Wasio wa kihandisi | 270 |
| **Jumla Ajira - Amali Zisizo za Kihandisi** | **6,186** |
| **Jumla ya Ajira - Amali** | **20,744** |
| Ujenzi wa Karakana | 11,500 |
| **Jumla - Amali** | **32,244** |
| **Jumla ya Uwekezaji** | **1,541,757** |
| **C. Uendeshaji** | |
| Utawala na Uendeshaji wa Shule na Vitabu (Mkondo Jumla na Amali) | 125,997 |
| Gharama ya Upimaji | 99,240 |
| Huduma- Mahitaji Maalum (Asilimia 0.25 ya uwekezaji) | 3,854 |
| **Jumla - Gharama za Uendeshaji** | **229,091** |
| **JUMLA KUU** | **1,770,848** |

## 6. Njia za Ugharamiaji

Ili kuhakikisha utekelezaji endelevu wa Elimu ya Lazima ya Miaka 10 bila kuathiri ubora wa elimu, ni muhimu kutumia mchanganyiko wa mikakati ya kifedha na kiutendaji. Mikakati hiyo ni pamoja na utumiaji kikamilifu wa miundombinu iliyopo, ikiwemo Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi; Vyuo vya VETA na Vyuo vya Ualimu na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi kupitia mifumo ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

### 6.1 Kutumia Miundombinu na Rasilimali Nyingine za Elimu

Ili kupunguza gharama za ujenzi wa miundombinu mipya ya shule, inapendekezwa kutumia miundombinu ya baadhi ya taasisi za Serikali zinazoweza kutoa elimu ya sekondari. Taasisi

hizo ni pamoja na Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC) na Vyuo vya Ualimu. Miundombinu inayowezakutumika ni pamoja na Madarasa, Karakana na Maabara.

## 6.2 Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi kupitia mifumo ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Kwa sasa, takribani asilimia **9.3** ya wanafunzi wote walio katika elimu ya sekondari hatua ya chini wanahudhuria shule zisizo za serikali. Ni dhahiri kwamba, ili sekta binafsi iweze kushiriki kikamilifu katika kupokea wanafunzi wa makundi-rika mawili, itabidi ifanye uwekezaji mkubwa ikiwemo upanuzi wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia na ajira mpya za walimu. Katika vikao baina ya WyEST, OWM-TAMISEMI na Sekta Binafsi, wadau wa sekta binafsi walipendekeza mikakati mbalimbali ya kushirikiana na Serikali katika utoaji wa elimu. Wadau walishauri ujengwe mfumo wa ushirikiano (Public-Private Partnership, PPP) wenye manufaa kwa pande zote.

Uchambuzi unaonesha kuwa, ili kufikia ushiriki wenye tija wa sekta binafsi, ni muhimu Serikali kuanzisha makubaliano rasmi ya kutumia miundombinu ya shule binafsi katika utoaji wa elimu ya sekondari. Wadau wa sekta hiyo wamependekeza mikakati mahsusi ikiwemo: Serikali kugharamia ada za wanafunzi katika shule binafsi; kutoa vocha (vouchers) zitakazomwezesha mwanafunzi kuchagua shule; na kukubaliana kuhusu gharama halisi ya kumpatia mwanafunzi elimu (student unit cost) bila kujali aina ya shule. Aidha, mifumo mingine ni pamoja na Serikali kutoa walimu na gharama za uendeshaji kwa shule binafsi; kutumia mifumo ya ujenzi na uendeshaji kama Jenga-Hamisha-Endesha (BTO), Jenga-Endesha-Hamisha (BOT), na Buni-Jenga-Fadhili (DBF); pamoja na kuanzisha Dhamana ya Miundombinu ya Elimu ya Samia (Samia Education Infrastructure Bond). Mifumo hii, ambayo chimbuko lake ni Sera na Sheria ya PPP, inalenga kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ya mwaka 2009.

Njia mbalimbali za ugharamiaji wa elimu ya lazima zimechambuliwa na Mapendekezo ya matumizi ya kila njia yametolewa kupitia Jedwali Na. 11.

***Jedwali Na.11:Jedwali la Uchambuzi wa  njia mbalimbali za ugharimiaji***

| Na. | Njia ya Ugharamiaji | Maelezo Mafupi | Nguvu (Strengths) | Changamoto (Weaknesses) | Mapendekezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Matumizi ya Miundombinu ya Umma (VETA, FDCs, Vyuo vya Ualimu, Shule za | Kutumia madarasa, karakana, na mabweni ya taasisi zilizopo (VETA, FDC na Vyuo vya Ualimu na Shule za Msingi) kutoa elimu ya sekondari. | Inaokoa fedha za ujenzi wa madarasa, karakana na mabweni muafaka kwa | Inahitaji uratibu wa matumizi ya pamoja (shared facilities) kati ya taasisi | Itumike katika kipindi chote cha mpito ili kupunguza idadi ya madarasa mapya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Msingi) | | mkondo wa Amali. | mama na wanafunzi wa sekondari. | yanayohitajiwa kujengwa. |
| 2 | Kulipia Ada Shule Binafsi | Serikali kulipa ada kwa wanafunzi wanaopangiwa shule binafsi (kipindi cha mpito). | Inatumia miundombinu iliyopo bila gharama za ujenzi mpya; Inapunguza msongamano haraka. | Hatari ya gharama zisizodhibitiwa na tofauti za ubora kati ya shule. | Itumike mijini ambapo ardhi ya kupanua shule za umma ni adimu. |
| 3 | Mfumo wa Voucher (Per-Student) | Fedha kumfuata mwanafunzi (Voucher) kwenda shule ya umma au binafsi. | Inaongeza chaguo kwa mzazi na kuchochea ushindani wa ubora wa shule. | Inaweza kuongeza pengo la usawa na kuchochea upandaji wa ada. | Serikali iweke thamani ya Voucher na kudhibiti ada kupitia mikataba na sekta binafsi. |
| 4 | Capitation Grant kwa Shule Binafsi | Serikali kulipa kiasi maalum kwa kila mwanafunzi aliyeandikishwa shule binafsi. | Inadhibiti gharama za Serikali; Ni rahisi kutekeleza kiteknolojia (ipo tayari shule za umma). | Huenda kiasi hicho kisitosheleze gharama halisi za shule binafsi. | Kurekebisha kanuni za Capitation ili kuhusisha shule binafsi zenye uwezo mdogo. |
| 5 | Ubadilishano (Walimu vs Majengo) | Serikali kutoa walimu na vifaa, shule binafsi kutoa majengo/miundombinu . | Inapunguza gharama za ujenzi kwa Serikali na gharama za uendeshaji kwa shule binafsi. | Changamoto za usimamizi wa walimu na migogoro ya uwajibikaji. | Mikataba iwe ya wazi na kuondoa utegemezi wa kudumu wa ajira za Serikali. |
| 6 | PPP za Miundombinu (BOT/BTO) | Ubia wa muda mrefu wa kujenga, kuendesha na hatimaye kukabidhi miundombinu kwa Serikali. | Inahakikisha uwekezaji endelevu na ubora wa hali ya juu wa majengo. | Inachukua muda mrefu kuandaa; Inahitaji uwezo mkubwa wa kitaasisi kusimamia. | Inafaa kwa miradi ya muda mrefu ya mabweni au vituo vikubwa vya ufundi. |
| 7 | Motisha za Kikodi | Kupunguza kodi au kutoa nafuu ya riba kwa wawekezaji wa | Inahamasisha sekta binafsi | Matokeo hayaji haraka (muda wa | Itumike kama kichocheo cha jumla cha |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | elimu. | kujenga shule mpya na kupunguza gharama za mitaji. | kati/mrefu); Serikali hupoteza mapato ya muda mfupi. | uwekezaji katika sekta ya elimu nchini. |
| 8 | Samia Education Infrastructure Bond | Dhamana ya muda wa kati/mrefu kukusanya mitaji kutoka soko la hisa kwa ujenzi wa miundombinu. | Inatoa fedha nyingi kwa mkupuo mmoja; Inaharakisha miradi mikubwa bila kusubiri bajeti ya kila mwaka. | Ni sehemu ya deni la umma; Inahitaji usimamizi madhubuti wa madeni na ufuatiliaji wa miradi. | Itumike kugharamia miradi mikubwa ya kitaifa na maeneo yenye msongamano mkubwa kuelekea 2028. |
| 9 | 2. Buni-Jenga-Fadhili (DBF) | Sekta binafsi inabuni na kufadhili ujenzi, Serikali inalipa kidogo kidogo baada ya mradi kukamilika. | Ni "accelerator" ya ujenzi wa haraka; Inapunguza shinikizo la papo hapo kwenye bajeti ya Serikali. | Inahitaji mfumo madhubuti wa uhakiki wa thamani ya fedha (Value for Money). | Iunganishwe na Samia Bond ili kupunguza gharama za mtaji na kuongeza kasi ya utekelezaji. |

### 6.2.1 Mapendekezo kwa Uteuzi wa Mfumo ya Ubia (*Decision Rules*)

Ili kushawishi uamuzi unaotekelezeka wa Mifumo ya ubia, inapendekezwa kutumia kanuni hizi za uteuzi:

i. **Mahitaji ya haraka ya nafasi (mwaka 2028) bila ardhi ya ujenzi (mijini)**: *Fee Subsidy* au *Unit Cost* kwa muda mfupi, ukiweka ceilings na masharti ya usawa/ubora inafaa kutumika;

ii. **Miundombinu mipya kwenye maeneo yenye ardhi/uwezo wa kujenga**: DBF (time-bound) au BOT/BTO (muda mrefu) kulingana na uwezo wa bajeti na hatari inafaa kutumika;

iii. **Kulinda usawa na kuepuka kuongeza mzigo kwa mzazi**: Mfumo wa voucher/fee utumike. Hata hivyo, taratibu za udhibiti wa ada na kanuni za kutokubagua zizingatiwe; na

iv. **Kulinda thamani-kwa-fedha**: mifumo yote ipitie taratibu za PPP na uthibitisho wa VfM/affordability kama inavyotakiwa kisheria.

## *7.* Mapendekezo ya Kipaumbele cha Afua kwa Kuzingatia Mtawanyiko na Msambao (Spatial distribution) wa Kiwango cha Msongamano wa Wanafunzi

Kwa kuzingatia uchambuzi wa Mtawanyiko na msambao, inapendekezwa kuwa:

i. **Kata 413 zilizoainishwa** katika kundi A na B zitumike kama msingi wa upangaji wa bajeti ya dharura kwa 2026/27;
ii. Halmashauri zilizo na idadi kubwa ya Kata hizi zipatiwe mgao mkubwa wa rasilimali;
iii. Mpango wa kushirikisha sekta binafsi uanze kwanza katika Kata za mijini na Miji ya Pembezoni (*peri-urban*);
iv. OWM-TAMISEMI isimamie upangaji wa rasilimali kwa kutumia orodha ya Kata kama kigezo rasmi cha maamuzi; na
v. Mamlaka za Serikali za Mitaa ziandae mipango ya utekelezaji ya ngazi ya Kata (*Ward-based implementation plans*).

## 8. Hitimisho

Utekelezaji wa Elimu ya Lazima ya Miaka 10 kuanzia mwaka 2028 ni hatua ya kimkakati katika mageuzi ya sekta ya elimu nchini. Hata hivyo, mafanikio yake yatategemea kwa kiasi kikubwa kiwango cha maandalizi ya utayari, hususan katika kipindi cha mpito cha makundi–rika mawili hadi mwaka 2031.

Andiko hili linaonesha kuwa mahitaji ya utekelezaji ni makubwa katika maeneo ya miundombinu, walimu, vifaa na fedha. Hivyo, utekelezaji wenye mafanikio unahitaji ushirikiano wa pamoja unaojumuisha Serikali, sekta binafsi, wadau wa maendeleo na jamii kwa ujumla. Kupitia maandalizi haya ya utayari, Serikali itaweza kuhakikisha kuwa lengo la kutoa Elimu ya Lazima ya Miaka 10 linatekelezwa bila kuathiri upatikanaji, usawa na ubora wa elimu kwa watoto wote wa Kitanzania.